**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**TAMKO LA SERIKALI KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI LITAKALOTOLEWA NA MHE. MHANDISI. HAMAD Y. MASAUNI (MB.), WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA, TAREHE 11 MEI, 2026**

**DAR ES SALAAM** **MEI, 2026**

***Ndugu Wanahabari,***

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na upendo kwa kutujalia zawadi ya uhai, afya na siha njema kukutana hapa siku ya leo. Aidha, kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais nawakaribisha katika kikao hiki kifupi cha kutoa Tamko la Serikali kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Kwa namna ya kipekee naomba niwasilishe salamu za upendo kutoka kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ambae anafahamu kuwa leo kupitia ninyi wadau wa Vyombo vya Habari Watanzania watapata kufahamu kauli, mwongozo na mwelekeo ya Serikali katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Aidha, Mheshimiwa Makamu wa Rais anathamini na kutambua mchango wenu mkubwa katika kuhabarisha na kufundisha jamii yetu kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi pamoja na Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

***Ndugu Wanahabari,***

Kama mnavyofahamu, tarehe 5 Juni kila mwaka nchi yetu huungana na Jumuiya ya Kimataifa katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku hii adhimu yaliasisiwa jijini Stockholm, Sweden, tarehe 5 Juni, 1972, wakati wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo ya Binadamu.

Lengo la maadhimisho haya ni kuelimisha na kuhimiza Jumuiya ya Kimataifa kushiriki katika shughuli za Hifadhi na Usimamizi Mazingira; kuchukua hatua za makusudi kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira pamoja na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali za Mazingira duniani kwa ajili ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

***Ndugu Wanahabari,***

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kimataifa kwa mwaka huu 2026 yatafanyika katika Jiji la Baku nchini Azerbaijan. Mtakumbuka kuwa Azerbaijan ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 29 wa Nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC - COP 29).

Kaulimbiu itakayoongoza maadhimisho haya Kimataifa ni **"Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Vitendo"**. Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa kuongeza kasi na juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesijoto, kukuza matumizi ya nishati mbadala, na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, kaulimbiu hii pia inahimiza Jumuiya ya Kimataifa kuchukua hatua za ziada na haraka za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimeendelea kujidhihirisha kupitia ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko, upungufu wa maji, kuibuka kwa magonjwa pamoja na kutishia usalama wa chakula duniani.

***Ndugu Wanahabari,***

Mbali na uwepo wa kauli mbiu ya kimataifa, tumejiwekea utaratibu wa kuwa na kaulimbiu ya kitaifa ambayo inaakisi vipaumbele vya Uhifadhi wa Mazingira pamoja na changamoto zilizopo ili kuendeleza juhudi za kukabiliana nazo. Hivyo kwa mwaka huu kaulimbiu ya Kitaifa ni **“Dira 2050: Tuwajibike kukijanisha Tanzania.”**

Kaulimbiu hii inahimiza jamii ya Watanzania kuchukua hatua za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Jitihada hizi lazima ziwe sehemu ya safari yetu ya maendeleo ya muda mrefu, ikiwa ni pamoja na kukijanisha Tanzania, kuongeza jitihada katika kulinda misitu yetu, na kupanda miti kwa wingi, ambapo asilimia 76 ya miti iliyopandwa kwa mwaka 2025/26 imestawi, kutumia nishati safi ya kupikia, ambapo matumizi ya nishati safi ya kupikia yameendelea kuongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 28.6 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia mwaka 2025.

Vilevile jitihada hizi zinahusisha kusimamia rasilimali kwa uendelevu, na kupunguza uchafuzi wa Mazingira ambapo, Tanzania huzalisha zaidi ya tani milioni 12.1 hadi 17.4 za taka ngumu kwa mwaka, ambapo inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia tani milioni 30-60 kwa mwaka ifikapo mwaka 2050. Aidha, asilimia 60 hadi 75 ya kiasi cha taka ngumu kinachozalishwa ni taka oza na asilimia 10-15 ni taka rejelezi (ikiwamo plastiki, karatasi, aluminiamu, glasi, taka za kielektroniki na chuma chakavu). Hivyo, kiasi cha taka oza kinachozalishwa kwa mwaka ni takribani tani milioni 9.9 ambapo ni asilimia ndogo tu hurejelezwa.

Kwa mantiki hiyo, kaulimbiu ya kitaifa inatafsiri kwa vitendo, wito wa kaulimbiu ya kimataifa kwamba, kila Mtanzania anapaswa kuchukua hatua sasa ili kuhakikisha kuwa maendeleo tunayoyapata hayaathiri mazingira na maisha ya vizazi vijavyo.

***Ndugu Wanahabari,***

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** imeendelea kuonesha dhamira thabiti kwa vitendo katika kutekeleza ajenda ya  Hifadhi ya Mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa vitendo. Kupitia sera ya Mazingira ya mwaka 2021 na mkakati wa utekelezaji wake, mikakati na mipango mbalimbali. Serikali inaendelea kuimarisha juhudi katika maeneo muhimu ikiwemo uhifadhi wa misitu kupitia kampeni endelevu za upandaji miti, kukuza matumizi ya nishati safi na mbadala, pamoja na kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Kupitia uongozi wa Mhesihimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchi yetu imeweza kupiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi pamoja na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi, hususan utekelezaji wa Miradi mikubwa ya kimkakati ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira

ambayo imewezesha Tanzania kutoa mchango katika jitihada za kikanda na kimataifa katika hifadhi ya Mazingira.

***Ndugu Wanahabari,***

Kama mnavyofahamu, siku chache zijazo, nchi yetu itaanza rasmi utekelezaji Dira ya Taifa ya maendeleo ya mwaka 2050 na Mpango wa Muda Mrefu wa Utekelezaji wa Dira *(LTPP, 2025 - 2050).* Aidha, Dira 2050 imetambua na kuweka mikakati madhubuti ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kupitia Nguzo ya Tatu inayohusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi, ambayo inalenga kufikia 2050 Tanzania iwe miongoni mwa nchi vinara wa utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira.

Kwa kutumia jukwaa la Siku hii ya Kielelezo ya Mazingira ya Duniani, natoa rai kwa wananchi wenzangu kuongeza kasi ya kuhifadhi Mazingira kwa kutekeleza shughuli mbalimbali kama vile: Upandaji na utunzaji miti; kuongeza kasi katika matumizi ya nishati safi ya kupikia, matumizi bora ya ardhi kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji pamoja kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya mazingira kwa umma. Vilevile, kuzingatia kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki kuhusu kuzuia uingizaji

nchini, usafirishaji nje ya nchi, uzalishaji, uuzaji, usambazaji, uhifadhi na matumizi ya mifuko ya plastiki.

***Ndugu Wanahabari,***

Katika kuadhimisha siku hii muhimu, tumepanga shughuli mbalimbali za kielelezo ambazo kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, napenda kuwaalika wadau wote na Wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika shughuli hizo. Shughuli zilizopangwa kufanyika kuelekea Maadhimisho ni kama ifuatavyo:

i. Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, **tarehe 11 Mei – 5 Juni, 2026;**

ii. Ushiriki wa viongozi na wananchi katika shughuli za kielelezo za upandaji miti na usafi wa mazingira katika Majiji nchini *(Arusha, Dar es salaam, Dodoma Mbeya, Mwanza na Tanga),* **tarehe 11 Mei – 5 Juni, 2026;**

iii. Upandaji Miti katika eneo la Bwawa la Kidete, Wilaya ya Kilosa, **terehe 15 Mei, 2026;**

iv. Kongamano la Vijana kuhusu Hifadhi ya Mazingira, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), **tarehe 26 Mei, 2026;**

v. Kongamano la Kisayansi na Utafiti wa Mazingira ambayo ni mojawapo ya shughuli za maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* pamoja na uzinduzi wa Kongamano la Wadau wa Mazingira *(Conference of Stakeholders on Environment (COSE),* Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNICC),* **tarehe 28 Mei, 2026;** Kongamano hili litahusisha washiriki takribani 1000 kutoka ndani ya Nchi, na nchi jirani za Afrika Mashariki;

vi. Maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNICC),* Dar es Salaam, **tarehe 29 Mei, 2026;**

vii. Maonesho ya teknolojia na ubunifu kuhusu shughuli za uhifadhi wa mazingira, Viunga vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, Dodoma, **tarehe 1 – 5 Juni, 2026;** Maonesho haya yatajumuisha wadau kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia, Vijana na Makundi mbalimbali. Aidha, maonesho haya yanatarajiwa kuwa na mabanda takribani 100.

viii. Uzinduzi wa Kituo cha Afrika cha Vijana cha Kujenga Uwezo wa Vijana kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, ushiriki

wao katika usimamizi na majadiliano katika majukwaa ya kimataifa (*African Youth Centre on Climate Change*).

ix. Uzinduzi wa Ofisi ya Kikanda ya Afrika ya Mfuko wa Upotevu na Hasara zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi (*Regional Office of the Santiago Network on Loss and Damage*).

x. Hafla ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani itakayofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, Dodoma, tarehe **05 Juni, 2026;** Mgeni Rasmi katika halfa hiyo anatarajiwa kuwa ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*****.** Katika hafla hiyo shughuli zitakazofanyika ni pamoja na: Uzinduzi wa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania (2026 – 2030), Programu hii ni nyenzo mahsusi ya kuwezesha utekelezaji wa Dira 2050 hususan nguzo inayohusu hifadhi ya mazingira na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi; na utoaji wa Tuzo za Maalum kwa wadau kutambua mchango wao katika Uhifadhi wa Mazingira.

***Ndugu Wanahabari,***

Kabla sijahitimisha tamko hili, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wanahabari na vyombo vya habari kwa kutumia muda wao kuhamasisha jamii kwenye masuala ya Hifadhi ya Mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zake. Aidha, nizishukuru pia Taasisi zote za Serikali, Asasi za kiraia na Asasi za kimataifa kwa kushirikiana na Serikali kufanya jitihada mbalimbali za kupambana na uharibifu wa mazingira.

***Ndugu Wanahabari,***

Mwisho, nitoe wito kwa Mikoa yote 26 nchini pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184, kushiriki kikamilifu katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa namna ambavyo wamejipanga pamoja kwa kushirikisha wadau pamoja na kutumia radio za kijamii zilizopo katika Halmashauri na Mikoa yenu kuhamasishana na kuelimisha jamii kwenye masuala yahusuyo hifadhi ya mazingira ikiwemo kutumia nishati mbadala wa mkaa, majiko banifu pamoja na kutumia njia sahihi za kuhifadhi taka. Tukumbuke kwamba, suala la Hifadhi ya Mazingira ni jukumu letu sote na tunapaswa kulitekeleza kwa vitendo.

*Mhe. Mha.* Hamad M.Y Massauni (Mb.),
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**